BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 22 Juni, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

1. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Biashara, Huduma za Jamii na Maeneo ya Kihistoria kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
2. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
3. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Taasisi za Umma kwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
4. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Nyumba za Biashara na Makaazi, Nyumba 370 za Fidia pamoja na Nyumba za Gharama Nafuu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
5. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Serikali na Ununuzi wa Vifaa vya Maabara ya ZBS kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
6. Ripoti ya Ukaguzi wa Mradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
7. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani pamoja na Ujenzi wa Viwanda vya Uchakataji na Usindikaji wa Dagaa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
8. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

9. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
10. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Vituo vya Afya na Nyumba za Wafanyakazi Unguja na Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
11. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
12. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Bandari na Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege (AAKIA Terminal 2-2), kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC):</u>

1. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Biashara, Huduma za Jamii na Maeneo ya Kihistoria kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
2. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
3. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Taasisi za Umma kwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
4. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Nyumba za Biashara na Makaazi Nyumba 370 za Fidia pamoja na Nyumba za Gharama Nafuu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
5. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Serikali na Ununuzi wa Vifaa vya Maabara ya ZBS kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
6. Ripoti ya Ukaguzi wa Mradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
7. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani pamoja na Ujenzi wa Viwanda vya Uchakataji na Usindikaji wa Dagaa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
8. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
9. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
10. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Vituo vya Afya na Nyumba za Wafanyakazi Unguja na Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
11. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
12. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa

Miundombinu ya Bandari na Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege (AAKIA Terminal 2-2), kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

## II. MASWALI:

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

462. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Hivi sasa Serikali ipo katika hatua za kukamilisha ujenzi wa kiwanja cha kimataifa kilichopo Fumba kwa ajili ya matumizi ya mashindano ya AFCON.

(a) Je, Serikali inaitumia vipi fursa ya ujio wa AFCON Zanzibar ili kuhakikisha Zanzibar wanakuwa wanachama wa kudumu wa CAF.

(b) Kwa kiasi gani Serikali imejipanga katika kuvisimamia, kuviendesha na kuviboresha (Maintenance Program) viwanja hivyo kabla na baada ya kumalizika kwa mashindano.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

479. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Sekondari Dkt. Shein iliyopo ndani ya jimbo la Wingwi, tayari imeongezewa madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa msingi.

(a) Je, ni lini madarasa haya yataanza kutumika.

(b) Kwa vile madarasa hayo yapo kwa muda mrefu sasa, ni lipi tatizo lililopelekea kutoanza kutumiwa.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

275. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Wete ilikuwa ni hospitali tegemezi kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba, lakini ghafla ilifungwa kwa lengo la kubomolewa na kujengwa kuwa ya kisasa. Hata hivyo, kwa muda mrefu ujenzi huo umekuwa ukisuasua hadi kuleta hofu na wasiwasi kwa wananchi wa Mkoa huo.

Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na ujenzi wa hospitali hiyo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

460. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Moja katika eneo linalowasaidia kiuchumi wakaazi wa Fuoni, ni eneo la Bonde la Mtwango na Kibonde Mzungu, kwa ulimaji wa Mpunga na mboga mboga, lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya uhifadhi wa maji.

Kwa nini Serikali haioni kama ipo haja ya kuwajengea bwawa litakalosaidia kuhifadhi maji watakayoweza kuyatumia kwa umwagiliaji katika kipindi cha Kiangazi.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

374. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Zoezi la kuitambua ardhi ya Zanzibar limekuwa la muda mrefu sasa, huku ikionekana wazi kuwa, maeneo mengi bado hayajatambuliwa na wananchi kupewa hati zao za Umiliki wa Ardhi.

(a) Hadi sasa, ni maeneo gani ambayo yameshatambuliwa na kusajiliwa ndani ya Zanzibar.

(b) Kwa nini maeneo mengi ambayo yametambuliwa na kusajiliwa mapema kama Nungwi, hadi leo bado hayajesha

kutambuliwa wala kusajiliwa huko.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

192. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Wazee, wajane na makundi maalum yenye uhitaji ni makundi yanayozidi kuongezeka katika jamii zetu. Hali hii hupelekea kuongezeka kwa utegemezi katika jamii na Serikali haionekani kufanya jitihada za kutosha za kuikabili changamoto hio.

(a) Kwa nini Serikali haianzishi mfumo (Data base) wa kuwatambua wajane wote wenye sifa kama wanavyotambulika wazee na Watu Wenye Mahitaji Maalum.

(b) Ni lini Serikali itasaidia kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa familia na malezi kwa wazanzibari.

(c) Je, Serikali ina mpango wa kuzuia ongezeko la omba omba katika Miji ya Zanzibar.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

154. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, kuna mpango gani wa kuongeza taa na alama za barabarani (Road sign) katika maeneo ya giza au hatarishi.

273. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Muda mrefu umepita hivi sasa tangu Serikali iliponunua mashine za MV. Maendeleo huko Mombasa nchini Kenya. Hata hivyo, Serikali ilipanga mashine hizo kuziuza lakini hadi sasa mteja hajapatikana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mashine hizo zinauzwa.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

186. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Vijana ndio taifa la leo na tegemezi kuu katika kukuza uchumi wa Zanzibar, ila kwa sasa changamoto wanazokumbana nazo katika utafutaji wa kujiinua na hali mbaya ya kiuchumi, huwapelekea kuishi katika mazingira hatarishi kwa kukusudia au kwa kutokukusudia.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuboresha miundombinu ya kumsaidia na kumlinda kijana wa kizanzibari, kutokana na hali mbaya ya mabadiliko ya dunia ya sayansi na teknolojia.

(b) Ni lini Serikali itaona haja ya kuwatumia mawakala wa ajira, kuwakusanya vijana kwa taaluma zao na kuwasambaza moja kwa moja katika miradi inayotekelezwa, ili kupunguza wimbi kubwa la ukosefu wa ajira.

(c) Ni lini Serikali italeta sheria ambayo itawalinda vijana wa kizanzibari wazawa, katika soko la ajira ndani ya nchi yao.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

182. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tarehe 10 Disemba ya kila mwaka, ni tarehe muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar, kwa sababu ndio tarehe iliyosajiliwa katika kumbukumbu za dunia kwa Zanzibar kupata uhuru wake kutoka kwa mkoloni wa Kiengereza.

(a) Je, kwa nini tarehe hii isitambulike rasmi na Serikali ili kuwawezesha mwananchi kujua jambo kubwa lililofanyika kwa maslahi ya Zanzibar.

(b) Je, kwa nini Serikali haioneshi jitihada zozote zile za kuienzi siku hii ya Uhuru wa Zanzibar.

(c) Ni lini Serikali itamtambuwa na kumuwezesha kupata heshima zake aliyekuwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Zanzibar, Marehemu Shekh Mohammed Shamte Bin Hamad.

472. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.:

Katika ulimwengu wa leo, dhana ya ushirikiano katika taasisi mbalimbali imepewa nafasi kubwa sana.

(a) Serikali inayatumia vipi Matamasha ya Utalii katika kuvitangaza viwanja vyetu vya ndege pamoja na vivutio mbali mbali vya utalii vilivyopo hapa Zanzibar.

(b) Kuna mashirikiano gani kati ya taasisi za Serikali katika kuifanikisha dhana ya utalii nchini.

## III. <u>KAULI ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

Hotuba za Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

1. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Biashara, Huduma za Jamii na Maeneo ya Kihistoria kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
2. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
3. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Taasisi za Umma kwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
4. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Nyumba za Biashara na Makaazi Nyumba 370 za Fidia pamoja na Nyumba za Gharama Nafuu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
5. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Serikali na Ununuzi wa Vifaa vya Maabara ya ZBS kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
6. Ripoti ya Ukaguzi wa Mradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
7. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani pamoja na Ujenzi wa Viwanda vya Uchakataji na Usindikaji wa Dagaa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
8. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
9. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
10. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Vituo vya Afya na Nyumba za Wafanyakazi Unguja na Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

11. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.
12. Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Bandari na Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege (AAKIA Terminal 2-2), kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**22 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR.**